JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO

6 JULAI, 2010

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 6 JULAI, 2010

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

MWENYEKITI WA KAMATI YA ARDHI, MALIASILI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa

Mwaka wa Fedha 2009/2010 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KUHUSU WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO PAMOJA NA WAZIRI WA KAZI, AJIRA NA MAENDELEO YA VIJANA:

Randama za Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo pamoja na Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011.

II. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

176. MHESHIMIWA WILLIAM HEZEKIA SHELLUKINDO (BUMBULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Kama inavyoonekana, Tume ya Uchaguzi inasimamia Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 1985 wakati inapotangaza Ratiba ya Uchaguzi Mkuu hadi kukamilisha utekelezaji:-

(a) Je, Sheria hiyo inasimamiwa na nani katika kipindi cha kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu au Mdogo hadi kipindi kingine cha Uchaguzi;

(b) Je, Wakuu wa Wilaya wanahusika vipi katika kuhakikisha kuwa Sheria za nchi ikiwemo Sheria ya Uchaguzi kwa ujumla hazivunjwi;

(c) Je, ni malalamiko mangapi ya ukiukwaji wa Sheria ya Uchaguzi yamewasilishwa katika Ofisi ya Waziri Mkuu kutoka kwa Wabunge na Vyama vya Siasa kwa ujumla.

177. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Mara kadhaa kumekuwepo na matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika Halmashauri mbalimbali na kusababisha kusuasua kwa maendeleo yaliyokusudiwa kwenye Halmashauri husika:-

Je, ni Halmashauri ngapi zimebainika na kero hiyo na ni wangapi waliohusika na kati ya hao ni wangapi wamechukuliwa hatua za kinidhamu katika kipindi cha kuanzia mwaka 2006 hadi 2010.

WIZARA YA MAENDELEO YA MIUNDOMBINU:

178. MHESHIMIWA VUAI ABDALLAH KHAMIS (MAGOGONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu:- Maeneo ya Msalato Mjini Dodoma ndipo kitakapojengwa kiwanja kikubwa cha ndege badala ya kiwanja kidogo kilichopo Dodoma Mjini sasa:-

(a) Je, upembuzi yakinifu unaofanywa sasa utamalizika lini.

(b) Je, ujenzi wa kiwanja hicho utaanza lini.

179. MHESHIMIWA SIRAJU JUMA KABOYONGA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Miundombinu:- Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na taarifa kuwa, Serikali inafanya matayarisho mbalimbali kuhusu ujenzi wa barabara za Nzega – Tabora na Itigi – Tabora – Kigoma pamoja na utafutaji wa fedha za kugharamia ujenzi wa barabara hizo:-

Je, Serikali inaweza kuliarifu Bunge hili kuwa, ni hatua gani imefikiwa mpaka sasa

katika utafutaji wa fedha zinazohitajika, na ni lini ujenzi wa barabara hizo mbili muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Tabora unatarajiwa kuanza.

WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

180. MHESHIMIWA JENISTA JOAKIM MHAGAMA (PERAMIHO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Suala la kuboresha kilimo ni pamoja na kuondoa jembe la mkono na kuleta kilimo chenye tija:-

(a) Je, ni lini Serikali itaamua kwa makusudi kutoa ruzuku maalum katika matrekta ya mkono, na majembe ya kukokotwa na wanyama na matrekta makubwa ili wakulima wayapate kwa bei nafuu na kwa urahisi;

(b) Mfuko wa Taifa wa Pembejeo bado hautoshelezi mahitaji ya maendeleo ya kilimo na hasa katika kusambaza zana bora za kilimo kwa wananchi;

Je, Serikali inalitambua hilo, na kama inalitambua inalitatuaje.

WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:

181. MHESHIMIWA PHILEMON MIKOL SARUNGI (RORYA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi:- Serikali imeonyesha dhamira ya kuendeleza Wavuvi nchini kwa kujenga mialo na kuendeleza mialo mingine na kuanzisha **BMU,** katika Wilaya ya Rorya kuna mialo 32 inayoendeshwa na wavuvi wanaoishi maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali itawasaidiaje Watendaji wa **BMU** kupata usafiri kama vile pikipiki;

(b) Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa mialo mingine 31 baada ya kukamilisha ujenzi wa **SOTA.**

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:

182. MHESHIMIWA JUMA HASSAN KILLIMBAH (IRAMBA MASHARIKI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi:- Upo mpango wa kuzifanya Shule za Sekondari za Lulumba na Iguguno Wilayani Iramba kuwa “High schools” Mpango ambao ulishakubaliwa na maandalizi yake yapo tayari pale Wilayani na Mkoani:-

(a) Je, Serikali inautambua mpango huo na ina mkakati gani kukamilisha hatua zilizobakia ikiwa ni pamoja na kuzitambua shule hizo;

(b) Je, kama mpango huo umepitishwa kwenye ngazi ya Wilaya na Mkoa, ni kwa nini utekelezaji wake haujaaanza;

(c) Wananchi wa Iramba Magharibi wamejitolea kujenga shule ishirini na tano (25) kwa nguvu zao; Je, Serikali itapeleka lini walimu hasa wa taaluma ya Sayansi ili kuunga mkono juhudi hizo za wananchi.

WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

183. MHESHIMIWA EMMANUEL JUMANNE LUHAHULA (BUKOMBE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Watumishi wanachama wa Mfuko wa Bima ya Taifa hudaiwa kupeleka *salary slip* zao tangu walipoingia Bima ya Taifa, punde mkataba unapoiva, hali inayoonekana kuwa ni usumbufu:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, huko ni kutowatendea haki wanachama hao;

(b) Je, kwa nini Serikali isiboreshe kumbukumbu zake ili kuzuia kumsumbua mwanachama wakati muda unapofika.

184. MHESHIMIWA MWADINI ABBAS JECHA (WETE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Uchumi:- Mashirika na taasisi nyingi za Umma zimekumbwa na matatizo mengi likiwemo la ukosefu wa mitaji ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya mashirika hayo:-

Je, Serikali iko tayari sasa kuanzisha Mfuko wa Umma wa Uwekezaji ili kukabiliana na tatizo hilo.

WIZARA YA NISHATI NA MADINI:

185. MHESHIMIWA HASNAIN GULAMABBAS DEWJI (KILWA KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Utafiti wa mafuta na Gesi uliofanyika katika Wilaya ya Kilwa Tarafa ya Pande eneo la Kisongo umesababisha kutengwa maeneo makubwa ambayo ni mali ya wananchi wa kijiji:-

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia zao.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa Mwaka wa Fedha, 2010/2011.

DODOMA
6 JULAI, 2010

DKT. T.D. KASHILILAH
KATIBU WA BUNGE